REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 12th November, 2025

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL

Speaker: Clerk, confirm whether we do we have quorum?

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: Without quorum, I direct that the bell be rang for ten minutes.

(The quorum bell was rang for six minutes)

Hon. Veronica Ikunyua: Mr. Speaker, I think we have got quorum now.

Speaker: Clerk, confirm if we do have quorum now.

(Clerk confirmed achievement of quorum)

Speaker: I direct that the bell stops ringing.

Hon. Nicholas Lempaira through Hon. Samuel Mugambi: Thank you, Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

NOTICE OF MOTION

ESTABLISHMENT OF LIVESTOCK REVOLVING FUND POLICY

Hon. Nicholas Lempaira through Hon. Samuel Mugambi: Hon. Speaker, I beg to give notice of the following motion;

THAT AWARE THAT livestock keeping is a major source of livelihood for a majority of residents in Laikipia County, especially in the arid and semi-arid areas;

FURTHER AWARE THAT livestock farmers continue to face recurring challenges such as prolonged droughts, outbreaks of livestock diseases, lack of affordable credit facilities, and fluctuating market prices, which greatly affects productivity and household income;

CONCERNED THAT recurrent droughts and disease outbreaks have led to massive losses of livestock, increased poverty levels, and food insecurity among pastoral and agro-pastoral communities;

NOTING THAT a Livestock Revolving Fund can provide sustainable financial support to farmers by offering low-interest loans or inputs for restocking, veterinary services, and feed acquisition;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

FURTHER NOTING THAT collaboration with established Savings and Credit Cooperative Societies (SACCOs) can ensure effective management, transparency, and accessibility of funds at the grassroots level; this House URGES the County Government to;

1. Establish a Livestock Revolving Fund aimed at providing affordable financial support to livestock farmers for purposes of restocking, purchase of animal feeds, and accessing veterinary services;
2. Collaborate with existing SACCOs and farmer cooperatives within the County to manage and disburse the funds transparently and efficiently; and
3. Develop clear guidelines and eligibility criteria to ensure equitable access and sustainability of the Fund for all livestock farmers across the County.

MOTION

ESTABLISHMENT OF LIVESTOCK REVOLVING FUND POLICY

Hon. Nicholas Lempaira through Hon. Samuel Mugambi: Hon. Speaker, I beg to move the following motion;

THAT AWARE THAT livestock keeping is a major source of livelihood for a majority of residents in Laikipia County, especially in the arid and semi-arid areas;

FURTHER AWARE THAT livestock farmers continue to face recurring challenges such as prolonged droughts, outbreaks of livestock diseases, lack of affordable credit facilities, and fluctuating market prices, which greatly affects productivity and household income;

CONCERNED THAT recurrent droughts and disease outbreaks have led to massive losses of livestock, increased poverty levels, and food insecurity among pastoral and agro-pastoral communities;

NOTING THAT a Livestock Revolving Fund can provide sustainable financial support to farmers by offering low-interest loans or inputs for restocking, veterinary services, and feed acquisition;

FURTHER NOTING THAT collaboration with established Savings and Credit Cooperative Societies (SACCOs) can ensure effective management, transparency, and accessibility of funds at the grassroots level; this House URGES the County Government to;

1. Establish a Livestock Revolving Fund aimed at providing affordable financial support to livestock farmers for purposes of restocking, purchase of animal feeds, and accessing veterinary services;
2. Collaborate with existing SACCOs and farmer cooperatives within the County to manage and disburse the funds transparently and efficiently; and
3. Develop clear guidelines and eligibility criteria to ensure equitable access and sustainability of the Fund for all livestock farmers across the County.

Hon. Speaker, this motion is about establishment of livestock revolving fund policy especially because the originator of the motion is Hon. Lempaira, representing Mukogodo West Ward. In Laikipia North, I know that the issues of livestock are the main economic activity.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

There is something that we should be talking about in Laikipia County on livestock especially to pastoralists and also to people who keep small number of livestock.

Laikipia County is one of the counties where we have the biggest livestock market in East Africa which is in Rumuruti. Hon. Speaker, when we have such things in our county, it is the highest time we get a revolving fund whereby those farmers and pastoralists gets access to the funds. The funds will help the farmers to restock and purchase animal feeds.

Hon. Speaker, yourself you are a pastoralist of bull fattening, I know that you learnt of bull fattening in Chicago either in primary or secondary. Even here in Laikipia, we should have such a programme whereby we know that in Doldol, Chumvi, Sosian or Segera we have got a bull fattening programme.

Hon. Lempaira wanted us to have an establishment of a revolving fund whereby we can be mapping some farmers and then they be given the livestock fattening programme and they be given an access to good market. Hon. Speaker, if you go to your record, in Kenya we don't meet the demand of meat in this country. So, I believe that this is a very good motion and also urge the Agriculture Committee to take over the motion and try and help us on how we can establish this revolving fund.

The motion also wanted us to collaborate with the existing Sacco's and farmer cooperatives within the county to manage and disburse the funds transparently and efficiently. It is very important so that these farmers can get facilities like loans whereby if a farmer has got a child in school, the farmer can educate his/her children using the revolving fund and also services from the Sacco's.

The third one, develop clear guidelines and eligibility to ensure equitable access and sustainability of the fund for all livestock farmers across the county. Maybe if you look at the National Government, they are doing a very important empowerment. However, these are also very important things to consider in the empowerment. Instead of giving them cash, maybe you should, for instance, go to Laikipia North and establish a revolving fund and give them that money. When the money is revolving, it is earning some interest which means that it is a sustainable source of livelihood for those people.

Having said that, Hon. Speaker, I want to call upon the Chairperson of the Finance Committee, Hon. Ndiritu. For the record, we come from the same ward. He was born in Salama, at an area called Muruku. He schooled there and later settled in Sweetwater's, Thingithu. So, we think along the same lines, because when you are born in the same area you think along the same lines. I have also visited his three farms. He is a rich person. He has a big farm in Umande, another one in Wamura and another very big farm in Sweetwater's. He solely does livestock farming. So, he understands these things better than us. So, let him not just second but also contribute to the debate about livestock. I now want to welcome him to second, thank you.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika. Nasimama kuuafiki mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Gatati. Huu ni mswada unaosema kuhusu mambo ambayo yanamhusu mwananchi kabisa. Sababu ya kwanza ya kuunga mkono ni kwa sababu aliyeuleta huu mswada ni Mheshimiwa Mugambi. Namjua Mheshimiwa Mugambi kama kijana ambaye anaona mbali, anayewafikiria wananchi na ambaye akili zake kila wakati zinafikiria jinsi ambavyo mwananchi atasaidika. Ndio maana nimesimama akili yangu yote ikiwa kwenye huu mswada.

Namshukuru sana kwa vile ameweza kuuleta, kuonyesha umuhimu, na kila Mbunge kwenye hili Bunge ameelewa nini kinachozungumziwa kwenye huu mswada. Mswada

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

hauletwi tu. Unaletwa, kujadiliwa na kuhakikishwa kuwa Wabunge wanauelewa. Bila hata kuongea mambo mengi, hata ambaye hajazungumza ataelewa ni kipi kilicho kwenye huu mswada kulingana na ulivyowasilishwa na ulivyosomwa.

Mheshimiwa Spika, huu mswada unaongea kuhusu mambo ya kuunda *revolving fund* ya mifugo. Tunapoongea kuhusu *revolving fund* ya mifugo, tunaongea kuhusu pesa ambayo itamsaidia mwananchi wa chini kabisa. Nilipoenda jandoni miaka mingi iliyopita, babangu alikuwa ameaga kitambo. Hivyo, mamangu alinipa mbuzi mmoja. Nilimtunza huyo mbuzi mmoja hadi wakafika kumi kufikiwa wakati nilikuwa nikitoka nyumbani hapo.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, *revolving fund* ni pesa itakayomsaidia mwananchi kuanza kutoka sufuri. Huu ni mswada ambao kila Mbunge anajua umuhimu wake, hususan sisi ambao tumechaguliwa na wananchi kuja kuwatetea. Jinsi ambavyo Mheshimiwa Mugambi amesema, mimi ni mkulima wa ng'ombe. Hiyo ndiyo kazi yangu ya ziada. Huu ni ukulima ambao wakulima wanahitaji usaidizi. Magonjwa, kiangazi na matatizo mengine yapo. Kwa hivyo, iwapo tutamsaidia mwananchi kupata fedha kidogo, ataweza kuhakikisha kuwa anapata pesa kwa haraka ya kumsaidia kwa mifugo anaofuga.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wana shida kadhaa. Mfugo anaweza kugonjeka asubuhi na kufikia jioni awe amewezwa. Kwa hivyo, mkulima anahitaji pesa kidogo ili mnyama akiwa mgonjwa anakimbia kwenye duka kununua dawa ili huyo mfugo apate matibabu na apone. Ndio maana tukiwa na hii pesa, itasaidia wananchi wote. Hatuzungumzi tu mambo ya Kaskazini kwenye hii fedha. Mimi niko Mashariki na nina ng'ombe. Kwa hivyo, ninahitaji hio *revolving fund.* Hio ni ya kila mwananchi ambaye ana hamu ya kufanya ufugaji.

Mimi kama mfugaji nimesajili wafugaji wengine. Sio mimi peke yangu, ninao wafuasi. Wajua, hata Yesu Kristo alikuwa na wafuasi. Ukiona mtu anayetembea peke yake, pengine ni mrogi. Kwa hivyo, ukifanya kitu mwonyeshe mwenzako. Mimi nina watu ambao nimewajulisha na wako hapa. Sitasema majina yao bali wanaelewa tunachokifanya. Ningetaka wengine wafuate kwa sababu hii ni njia moja ya kuhakikisha kuwa tunapata pesa mfukoni.

Wengi hapa tulichaguliwa kwenye chama cha UDA, ingawa baadaye tuliwaleta wenzetu wa ODM tukae pamoja kwa sababu Kenya ni kubwa na ni yetu sisi sote. Tuliingia na roho ya *bottom-up.* Hilo ni jambo la kumwinua mwananchi kutoka chini na kumleta juu. Juzi tuliona *empowerment* ambapo serikali ya kitaifa inaenda mashinani na kuwapa watu pesa. Ukinipa elfu mia moja sasa hivi, hio sio *empowerment.* Hio ni pesa ya matumizi. Bali ukinipa *revolving fund* ya mifugo nitaenda kununua ng'ombe. Huyo ng'ombe atanipa mbloea, maziwa na nyama. Hivyo vitu vyote vitatu vitanisaidia. Nitaweka mbolea kwenye shamba. Mimea mingine na chakula cha ng'ombe yatatunzwa. Nitauza maziwa watoto wasome.

Hii mia mbili mnayonipa hapa ni kidogo sana na ni pesa ambayo haitamsaidia mwananchi. Sisemi ni vibaya tukipewa. Tupewe tu kwa sababu hii ni pesa ya serikali. Ni kama kutolewa pesa kwenye huu mfuko wangu na kuweka kwenye huo mwingine. Ni pesa yangu tu, ni vile tu haijapangwa vizuri. Mimi nakubaliana nao katika uwezeshaji wa watu wetu. Hata hivyo, iwe kwa njia inayofaa na itakayowasaidia wananchi. Kwa hayo machache, naunga mkono huu mswada na kuwaomba Wabunge wengine kuunga mkono huu mswada ili angalau mambo yafanywe na wananchi wetu wasaidike.

Pili, Mheshimiwa Spika, mswada unasema "*collaborate with existing saccos.*" Sio kwamba hii pesa itachukuliwa tu na kepeanwa huko. Itapeanwa kwenye sacco na mkulima atafute hiyo pesa hapo. Vilevile, unasema "*develop a guideline and eligibility criteria to ensure equitable access.*"

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Equitable access ni kuumanisha kila mtu aweze kufikia hizo pesa ukiwa mzee, kijana, mama ama umri wowote. Hii si pesa ya wazee, vijana ama akina mama kama inavyosemekana. Hii ni pesa yetu. Sisi wote tuweze kufikia pesa kwa njia ambayo inafaa. Kwa hayo machache, ninaunga mkono na kuafiki huu mjadala wa Mheshimiwa Samuel Gatati.

Vilevile Mheshimiwa Mugambi amesema nimetoka Salama ambapo ni kweli. Sisi watu ambao tumetoka huko tunaangalia sana maneno. Ninamkumbusha ya kwamba nilihama Salama na sasa niko Thingithu. Asinipigishe vita kwa kusema niko Salama. Nilitoka kwa sababu tulizaliwa na tumekuwa wakubwa wa kwenda kutafuta kama wanaume mwingine ndiposa tukapatana hapa.

Yeye ni Mheshimiwa kutoka Salama na kesho kutwa ninataka kusikia akiwa Mbunge wa Mashariki mwa Laikipia, Waziri katika Kaunti yetu na akiwa na mambo makubwa kwa sababu watu wa Salama tunatoka chini tukielekea juu. Asante, Mheshimiwa Spika.

Speaker: Thank you, Hon. Mugambi and Hon. Stephen. Now, the establishment of livestock revolving fund policy's motion has been moved and seconded.

(Question proposed)

Hon. Salim Edung: Ninashukuru sana Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi ili niunge mkono mswada wa leo ambao umeletwa na Mheshimiwa Gatati ambaye anawakilisha Mheshimiwa Lempaira. Kuhusu Wanyama ambao tunahitaji katika Laikipia, kuwa na *revolving funds* itakuwa njia moja ya kutusaidia katika Laikipia yetu. Malengo ni upande wa ufugaji.

Ukiangalia *ranchers*, wananchi wengi wamekaa pamoja na *ranchers* na kujadiliana jinsi ya kuweka ng'ombe kwenye hizo mashamba, wakuze na watakaponona waanze kuuza. Hiyo ni njia moja ya kusaidia wananchi katika Laikipia kwa mapato. Hii imesaidia wananchi kwa sababu ng'ombe inaponona, wenye ranchi wanaita wenye ng'ombe na kusikizana bei. Kutoka hapo wenye ranchi wananunua.

Hii ni njia moja ya kusaidia yule mwananchi ambaye yuko mashinani kwa sababu anaweza kuzunguka na ng'ombe lakini anakosa mahali pa kuuza hiyo ng'ombe. Katika *revolving fund,* vijana watasaidika. Wanapopata pesa, wanafanya biashara. Wanatembea katika kila soko na kununua ng'ombe wakiuza.

Bila hiyo pesa, hao vijana watakosa kazi ambayo tunasema ya kwamba ni lazima tuinue vijana walio mashinani na vijijini ili wapate kazi. Huu mswada utasaidia watu wengi sana. Kama vile asubuhi tulikuwa na mjadala wa maziwa, adhuhuri tumeona kuna mswada kuhusu ng'ombe ili wasaidie wananchi kwa kununua na kuuza. Hii ni njia moja ya kusaidia vijana ili wawe wanafanya kazi kwa sababu wanasema hakuna kazi.

Anapopata pesa kutoka kwa hii hazina ya kuinua watu walio chini kwa kuchukua pesa kutoka Sacco na waiweke mahali ili wauze wapate pesa. Hii inaonyesha ya kwamba kuna hatua tunapiga katika Kaunti yetu. Tunajali wakulima wa hawa Wanyama. Kwa hayo machache, ninajua huu mswada haukuletwa kufurahisha mtu bali uliletwa ili utekelezwe na usaidie wananchi wa Laikipia. Asante Bwana Spika.

Hon. Catherine Kibue: Asante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza namshukuru mwenye ametusomea huu mswada, kijana barubaru; Mheshimiwa kutoka Wadi ya Salama. Bwana Spika, kama kuna siku inafaa kubaki kwenye historia katika hili Bunge ni siku ya leo. Uhakika ni kuwa viongozi katika hili Bunge wamefanya uwezeshaji kwa wakulima wetu. Ninaona mswada ambao tulikuwa tunajadili asubuhi ni kama wa sasa. Asubuhi tuliongea

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

maneno ya maziwa na saa hii tunaonyeshwa kule ambapo tutapata pesa ili tuweze kuongeza mifugo yetu.

Kwa uhakika kama kuna jambo tumefanya hata kama Mheshimiwa kutoka Salama anasema alihama, kama kuna jambo tumefanya la kusaidia wananchi wa Laikipia ni sasa hivi. Hii ni kumaanisha tunavyotumia wananchi wetu, hatutaweza kuwatumia kwa sababu watakuwa na kazi zao. Tukiwapa hizi pesa wataangalia mifugo yao. Bwana Spika, hata kama ni zawadi tulikuwa tunapatiana siku ya leo ningepatia mwenye mswada ama hili Bunge kwa kuona uhakika wa kuangalia wananchi wetu.

Pia, sisi viongozi ambao tuko hapa hata kama tunatetea wananchi wetu, tuige mfano wa Mheshimiwa A.K.A Kagondu atulee ili hii pesa ikikuja kwa sababu haiangalii umri ama jinsia. Kwa hivyo, itatuinua na tuweze kuongeza mifugo.

Kwa hivyo sisi wenye tumekuwa wanafunzi wa Mheshimiwa Kagondu nikiwa mmoja wao, naomba wengine na vijana barubaru wenye waliambiwa wanazaa sana muweke mifugo mingi ndio muweze kusomesha watoto na kuwainua. Naunga mkono na naomba wenzangu tuwe tunatetea wananchi wetu na kufanya kitu ambacho kesho na kesho kutwa kitakuwa cha kukumbukwa. Asante.

Hon. Benson Kuria: Asante, Bwana Spika kwa fursa hii ambayo umenikabidhia. Pia nashukuru kwa mswada ambao tumepewa na Mheshimiwa Gatati. Naona kuna jina ameongezewa kwamba mwaka wa 2032 awe mjumbe katika Laikipia Magharibi. Itakuwa baraka. Huu ni mswada wa mzunguko wa hera mifukoni. Nikilinganisha na mswada wa asubuhi wa maziwa katika jimbo letu la Laikipia. Ni kama alikuwa ameangalia kitabu cha 1 Samueli 17; *'inasema wakati Daudi alikuwa anajipanga kwa sababu alikuwa mfugaji nabari moja. Alipoambiwa avalie mavazi ya sauli, alisema hawezani nayo.'* Huu ni mswada unaonyesha kwamba katika jimbo letu la Laikipia, lengo kuu sana sana ni ufugaji.

Ukiangalia mzunguko wa soko kuanzia siku ya Jumatatu hadi Jumapili, watu huzunguka na mauzo ya mali. Hizi pesa zikiingia mifuko na ziwe na mipangilio mzuri ni kumaanisha waakilishi wa Laikipia baraka ziko juu yao kutoka kwa mwenyezi Mungu. Kumaanisha pesa zikizunguka, hakuna mtu ataweza kuwa maskini ama mwizi ama mporaji kwa maana kuna mtu anamfikiria.

Ndiposa niko hapa kuwakilisha jimbo la Laikipia na Chama cha UDA na kuunga mkono mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Gatati ambaye ni kijana Gen-Z na hajawahi kosa Bunge. Namuombea aishi siku nyingi. Afikishe miaka kama yangu 68 sasa. Nashukuru. Nikiulizwa katika Bunge la Laikipia ni mjumbe mgani ameleta miswada mingi katika Bunge nitasema ni Mheshimiwa wa Thingithu na hivyo ndivyo kulivyo. Asante nashukuru na naunga mkono.

Speaker: Thank you, Honourable Benson. Allow me now to call upon the mover of the motion to reply.

Hon. Samuel Mugambi: Thank you, Hon. Speaker. I want to congratulate the Hon. Members who have given us a serene and robust conversation about the establishment of a livestock-revolving fund in Laikipia County. I want to congratulate my seconder Hon. Kagondu who comes from the same ward but now represents the people of Thingithu. I also want to congratulate Hon. Nyokabi who is my immediate neighbour. What happens in Ngobit happens in Salama. In fact, we even share church priests. You understand that a priest in AIPCA who preaches in Salama also preaches in Ngobit. Ngobit and Salama is like one ward.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

I also want to congratulate my senior, my elder brother, Hon. Kamara who we share a lot and we have a history with him. If Laikipia Assembly history will be written in my life, Hon. Kamara will take a chapter. We have a very long history with Honourable Kamara from where we come from. Our origin in politics and so many other things about Kikuyu culture and so many things that we share. All other Members who have contributed, Hon. Salim who is also my neighbour there. We neighbour with ADC Mutara Farm. Between Segera and Salama is ADC Farm.

So when you cross ADC Farm, you're in Mutara, you're in Salama. When you go to the other side, you're in Segera. We share a lot. We have a location called Thome which is made up purely the of Turkana community. And they voted for me 90%. So I'm a great friend of Turkana. When I hear of these Members telling me of getting more children, I think they are not supposed to be telling me to get more children. They are supposed me to get more wives for me to get more children.

I think one of these days I should get a Turkana wife and get more children. What Honourable Kamara is praying for me to become the Member of Parliament for Laikipia East constituency. Hon. Kagondu is telling me to become a member of Laikipia East constituency. I would like to become a member of Laikipia West. Because my ward is geographically is Laikipia West. But also is the middle of Laikipia East and West.

So thank you, Hon. Speaker. I also want to congratulate you for your intelligence and your intelligence in every move we make as an Assembly. You are moving very well. If you continue this way, we shall do a party for you. Thank you, Hon. Speaker and I thank the Honourable House.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until 18th of November, 2025 at 10.00 a.m.

The House rose at 3.22 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*